KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI



# Ujuzi wa Kusoma na Kuandika Kifedha

## Usimamizi wa Biashara na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika wa Kidijitali kwa Wanawake Wajasiriamali Wadogo

*Ripoti hii imeweza kufanikishwa kwa ushirikiano wa ukarimu na watu wa Marekani kupitia Uwakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Muongozo huu ulitolewa chini ya Mradi wa Frontia za Kidijitali za DAI (Cooperative Agreement AID-OAA-A-17-00033) kutokana na ombi la USAID wakishirikiana na Mastercard.*

# Taaswira ya Moduli

## Jedwali la yaliyomo


**Sehemu ya 1:** Ufunguaji wa Akaunti ya Kifedha 5

**Sehemu ya 2:** Akiba 11

**Sehemu ya 3:** Kufanya Bajeti 22

**Sehemu ya 4:** Uwekezaji 29

**Sehemu ya 5:** Bima 33

**Sehemu ya 6:** Mkopo 40


## Malengo

Elewa jinsi ya kuweka akiba, kutumia, au kuongeza pesa zako.

## Kwenye Moduli hii, unaweza.....

- kulinganisha na kubainisha aina tofauti za akaunti za kifedha na watoaji huduma
- kutengeneza bajeti yako mwenyewe.
- kuangalia nafasi za uwekezaji wa biashara yako
- kutathmini gharama na faida za bima.
- kujifunza kuhusu majukumu ya mkopo katika biashara



Kwanza, hebu tutathmini jinsi unavyosimamia fedha zako!
Nani kati yenu hapa mwenye akaunti ya akiba katika benki au anaweka akiba kwenye pochi zenu za simu? Ikiwa hakuna, mnafanyia nini pesa zenu?
Ni aina gani za bima una ufahamu nazo?
Ni wangapi kati yenu wanaofanya bajeti za fedha za biashara zao?

# SEHEMU YA 1: UFUNGUAJI WA AKAUNTI YA KIFEDHA

**Malengo:**

1. Kuelewa jinsi ya kufungua akaunti kwa mtoaji huduma wa kifedha.
2. Kujifunza kuhusu aina ya stakabadhi mahsusi zinazohitajika ili kukuwezesha kufungua akaunti.



# Kufungua Akaunti kwa Watoaji Huduma za Kifedha



**Kufungua akaunti kwa mtoaji huduma wa Kifedha – kama vile benki au mtoaji huduma wa pochi ya simu – wanatoa faida nyingi kwenye biashara yako. Unaweza kuitumia akaunti hiyo kuweka akiba au kuwekeza pesa, kufuatilia mapato yako na matumizi, kulipa wasambazaji wako, na pia kukuwezesha kupata mkopo.**

Ukiwa na akaunti, utakuwa na rekodi za shughuli zako za kifedha ili kusimamia biashara yako na kutabiri mapato yako ya baadaye.

Unaweza kufungua akaunti tofauti za kifedha ili kumudu mahitaji yako. Kwa mfano, akaunti ya akiba ili kukusanya pesa kwa malengo maalumu – kama vile kununua jokofu kwa duka lako – au akaunti ya kuangalia matumizi ya kila siku, kama vile kulipa bili au kununulia bidhaa.

# Nafungua vipi Akaunti?

1

**Fanya utafiti wako.** Sio watoaji huduma wote wa kifedha wanaotoa huduma na bidhaa sawa. Ni muhimu kuwa na ufahamu wa huduma unazotaka kabla ya kuchagua mtoaji huduma na aina ya akaunti unayotaka kufungua.

2

**Jua ni wapi unapotaka kwenda ili kufungua akaunti.** Wakati mwingine, unaweza kutuma maombi ya kufungua akaunti mtandaoni au kwenye simu yako. Watoaji huduma wengine wanaweza kukuhitaji ufike wewe mwenyewe binafsi.

3

**Kusanya stakabadhi zinazohitajika.** Stakabadhi zinazohitajika zinategemea na mtoaji wako wa huduma za kifedha. Kwa hakika, utahitajika kuwa aina ya utambulisho na ithibati ya anwani.

4

**Kujaza fomu ya maombi.** Pindi utakapokuwa na stakabadhi zinazohitajika, unaweza kumalizia kujaza fomu ya maombi ya akaunti.

5

**Anza kutumia akaunti yako.** Pindi maombi yako yatakapoidhinishwa, unaweza kuanza kutumia akaunti yako kwa mahitaji yako yote ya kifedha!

# Akaunti za Biashara na za Kibinafsi

Ukiwa mjasiriamali, unahitajika kuwa na akaunti tofauti za fedha, za biashara yako na za kibinafsi. Hizi ni baadhi ya sababu:

**Kufuatilia kwa urahisi na usahihi kuingia na kutoka kwa pesa za biashara yako.** Ukiwa na akaunti tofauti za kibinafsi na biashara, unapata taaswira sahihi ya hali ilivyo ya fedha za biashara yako. Hii itakusaidia kuelewa jinsi ambavyo biashara yako inaendelea kila wakati, na kukuwezesha kutabiri hali ya baadaye ya pesa zinavyoingia na kutoka.

**Kukinga mali zako za kibinafsi.** Ukiwa na akaunti tofauti inaweza kukusaidia kushughulikia biashara yako kujisimamia kivyake, wakati unalinda mali zako za kibinafsi dhidi ya matatizo kwenye biashara.

**Kupata manufaa ya faida za kodi.** Ankara zako zote na shughuli za kifedha zitaathiri jinsi utakavyo lipa kodi. Wenye biashara na wajasiriamali wanaweza kupata baadhi ya faida za kodi, kwa hivyo ukiwa maelezo yote pamoja yanayohusu biashara yako, yanaweza kukusaidia kuokoa muda mwingi na pilka pilka za hapa na pale.


Kila mwanamke anahitajika kuwa na akaunti binafsi ya benki?
Kuna hatari zipi ikiwa mwanamke hata akaunti yake mwenyewwe?
Ni wangapi kati yenu wenye akaunti zao wenyewe za benki? Unaitumia kufanyia nini? Unaiendesha mwenyewe?
Ni wangapi kati yenu mnaoshirikiana au kuendesha akaunti ya benki na mtu mwengine?

# Kwanini Nahitajika Kuwa Na Akaunti Yangu Mwenyewe?



Kwa kuwa baadhi yenu mnaweza kuwa hamna akaunti zenu wenyewe kwa mtoaji huduma za kifedha, sasa tueleze kwa kina faida za kufungua akaunti kwa jina lako.

1. **Kusimamia fedha zako binafsi na za biashara.**
   Kufungua akaunti kwa jina lako inakupa nafasi ya kutenganisha fedha zako binafsi na za biashara. Utakuwa unaweza kupokea mshahara wako kutoka kwa biashara yako na malipo kutoka kwa wengine hadi kwa akaunti yako.

2. **Kuwa na ujuzi wa kifedha.**
   Ukiwa mjasiriamali ni muhimu kuwa na ujuzi wa kifedha, kwasababu unahitajika kuwa na ufahamu wa istilahi tofauti za kifedhana mikakati. Kufungua akaunti yako mwenyewe kutakupa ujasiri wa kutumia bidhaa na huduma tofauti.

3. **Kuwa na uhuru wa Kifedha.**
   Ukiwa na akaunti yako mwenyewe, unakuwa na uhuru wa kuamua jinsi ya kuweka akiba, kutumia na kuwekeza pesa zako. Unaweza pia kuchukua hatua ya kujikinga mwenyewe kukitokea janga au jambo la ghafla – ni kama kuweka hazina yako ya dharura.

# SEHEMU YA 2:
# AKIBA





## Malengo:

1. Kuweza kujua thamani ya kuweka akiba.
2. Kujifunza jinsi ya kufanya maamuzi ya kimkakati kwamba ni shilingi ngapi na ni wapi utaweka akiba.

# Sasa tuzungumze kuhusu akiba

**Akiba ni kile ambacho kinabaki kutokana na mapato yako baada ya kulipia matumizi yako muhimu na yasiyo muhimu.**



# Kwanini ni Muhimu Kuwa na Akiba?



Kupangilia matumizi ya baadaye



Kutengeneza hazina ya dharura



Kujenga utajiri wako



# Mahitaji na. Yanayotakiwa



## MATUMIZI MUHIMU NA YASIYO-MUHIMU

**MAHITAJI** ni mambo ambayo ni lazima uwe nayo, kama vile chakula au kodi ya nyumba yako au biashara. Yanahitajika ili kukupa utulivu na hali njema ya kimwili na kisaikolojia.

**MAHITAJI ni muhimu.**

**YANAYOTAKIWA** ni mambo ambayo unatamani kuwa nayo, nguo za mitindo au rangi ya duka lako. Ni vitu vya kununua ambavyo havihitajiki ili kukufanya uishi, lakini ungependa kuwa navyo.

**YANAYOTAKIWA ni yasiyo-muhimu.**




# Nahitajika Kuweka Akiba Ya Shilingi Ngapi?

**Wataalamu wanapendekeza kuwa wakati wowote lazima kwenye akiba ya familia kuwe na kiwango cha pesa ambacho kinaweza kukidhi matumizi ya mahitaji yao muhimu angalau kwa miezi sita.**

Inazingatiwa kuwa ni mazoea mazuri kuweka akiba angalau ya asilimia 20% ya mapato ya familia, ukichukulia kwamba asilimia 50% itatumika kwenye matumizi muhimu (kama vile chakula na kodi ya nyumba) na asilimia 30% itumike kwenye matumizi mengine ya hiari.

Pia unahitaji kuzingatia kuweka akiba ya matumizi ya biashara yako. Biashara zinahitajika kuweka akiba ili kuweza kulipia matumizi ambayo hayakutarajiwa, kama vile kutaka kubadilisha jokofu au kitabu cha rekodi cha dukani.



# Ni Vipi Naweza Kuweka Akiba Nikiwa Na Mapato Machache?



- Anza kwa kuweka akiba ya kiwango kidogo cha pesa.
- Fanya kuweka akiba kuwa tabia yako ya kila mara.
- Weka akiba zako mahali pazuri na penye usalama.
- Chagua akaunti ya akiba ambayo itakuwa riba.
- Pitia matumizi yako na ondoa matumizi ambayo sio muhimu.

# Akiba Rasmi




**Wakati unaweka akiba zako kwenye mashirika au taasisi, kama vile benki, utakuwa unaweka akiba kwenye mfumo rasmi wa kifedha.**

Mifano ya taasisi rasmi za kifedha ni benki, taasisi ndogo ndogo za mikopo, watoaji huduma wa pochi ya simu kama vile waendeshaji wa mitandao ya simu, na vyama vya mikopo.

Ukitumia mfumo wa akiba rasmi, pesa zako zitakuwa zinalindwa vizuri. Serikali na taasisi zingine huwa zimeweka kanuni na sheria ambazo taasisi rasmi zinahitajika kufuata kuweka pesa zako salama.

Akiba rasmi zinazalisha, kumaanisha kuwa unaweza kupata riba kwenye pesa zako. Wewe angalia ada!

# Aina za Akaunti za Akiba Rasmi

Kuna aina nyingi za akaunti za akiba unazoweza kuchagua. Hebu tueleze baadhi zinazoweza kupatikana kwako!

**Akaunti za akiba za kitamaduni.** Akaunti za akiba za kitamaduni ni akaunti za kawaida! Hizi akaunti ni zile ambazo unaziona kwenye benki au vyama vya mikopo. Akaunti za akiba za kitamaduni ni nzuri kwa wale wanaoingia kwenye mfumo rasmi wa kifedha kwa mara ya kwanza.

**Akaunti za kujiwekea masharti ya akiba.** Akaunti za kujiwekea masharti ya akiba zinakupa nafasi ya kukuzuia wewe kutumia akiba yako mpaka tarehe maalum uliyoweka ifike au kifike kiwango ulichoweka kutimiza lengo lako. Hizi akaunti zinakupa motisha wa kuweka akiba, kwa kuwa huwezi kuzitumia pesa zako mpaka malengo yako yatimie.

**Akaunti za utaalamu za kuweka akiba.** Akaunti za utaalamu za kuweka akiba zimetengenezwa ili kukusaidia wewe kufikia malengo tofauti unayoweza kuwa nayo. Kwa mfano, unaweza kuwa na akaunti ya utaalamu ya akiba ambayo imetengenezwa kwa ajili ya masomo ya mwanao au yako wewe utakapo staafu.

# Akiba Zisizo Rasmi



**Mfumo wa akiba zisizo rasmi ni njia tofauti ambayo watu wanaweka akiba tofauti na mfumo wa akiba rasmi. Tofauti na akiba rasmi, mifumo ya akiba zisizo rasmi huwa hazina kanuni wala sheria za kufwatwa.**

Mifano ya mifumo ya akiba zisizo rasmi ni miungano ya mikopo na vijiji, vinavyoweka akiba kwa zamu na miungano ya mikopo, na vikundi vya kujisaidia wenyewe kwa wenyewe. Kuweka akiba kwenye mkebe au kisanduku pia ni mbinu ya kuweka akiba zisizo rasmi.

Sheria za kushiriki kwenye kikundi cha kuweka akiba kisichokuwa rasmi huwa zinaamuliwa na wanachama. Zinaweza kupatikana na kurekebishwa baada ya muda, kulingana na mahitaji ya wanachama.

# Ni Mfumo Gani wa Kuweka Akiba Nahitajika Kuchagua?

Mifumo yote ya akiba rasmi na zisizo rasmi hutumika sana ulimwenguni. Hapa kuna baadhi ya mambo ya kuzingatia wakati unafanya maamuzi ya aina ipi ya uwekaji akiba unaokufaa.

| AKIBA ZISIZO RASMI | AKIBA RASMI |
|---|---|
| • Akiba zisizo rasmi mara nyingi zinakubalika vizuri kwenye maisha ya watu; ukiweka akiba kwenye kikundi cha uwekaji akiba, sheria zitakuwa zinalingania utamaduni na mahitaji ya kikundi. Wanachama wanaweza kurekebisha uendeshaji wa kikundi unapohitajika.<br>• Akiba zisizo rasmi mara nyingi hutoa thamani zaidi ya huduma za kifedha. Kwa watu wengi, kukutana na kikundi chao cha kuweka akiba ni njia ya mtagusano mzuri.<br>• Vikundi vya akiba zisizo rasmi vinaweza kukosa rekodi za kuaminika za shughuli za akiba.<br>• Kuna vipengele vichache vya usalama wa kulinda pesa zako kwenye mifumo isiyo rasmi ikilinganishwa na mifumo rasmi. | • Wakati mwingine mifumo ya akiba rasmi haitoi urahisi na faida zisizokuwa za kifedha zinazotolewa na mifumo ya akiba zisizo.<br>• Taasisi rasmi za kifedha zinaweza kutoa huduma ambazo mifumo isiyo rasmi haiwezi, kama vile kuweka akiba binafsi, kuweka akiba ya kiwango kikubwa cha pesa, kuweka akiba kwa kipindi cha muda mrefu, na usalama wa pesa zako.<br>• Taasisi yako rasmi ya kifedha itakuwekea stakabadhi za rekodi za shughuli zako na akaunti, ambazo unaweza kuzifikia na kutumia unapohitaji. |

# Kuweka akiba na Hey Sister




**Masomo ya Hey Sister**


Somo la 15: Niweke akiba ya shilingi ngapi?

Somo la 16: Niweke akiba wapi?

# SEHEMU YA 3: KUFANYA BAJETI

**Malengo:**

1. Kufahamu vidokezo vya kutumia kufanya bajeti.
2. Kufanya bajeti yako mwenyewe ya kawaida.



# Kufanya Bajeti


**Kufanya Bajeti ni mchakato wa kufuatilia mapato na matumizi yako.**

Kufanya bajeti kunakusaidia kuamua kuwa pesa zako utazitumia wapi. Kawaida, unafanya bajeti ya mapato na matumizi yako kila mwezi, lakini pia unaweza kufanya bajeti za kila wiki au hata mwaka.

Ukiwa mjasiriamali, kufanya bajeti kunaweza kukusaidia wewe kufuatilia fedha zako za nyumbani na biashara. Unaweza pia kutengeneza bajeti ili kukusaidia wewe kufikia malengo yako ya kifedha ya muda mfupi na muda mrefu.



# Mipango ya Kifedha: malengo ya muda mfupi na muda mrefu




## Malengo yako ni yapi?

### Malengo ya Muda Mfupi

Mfano: Kununua jokofu la dukani kwako.

### Malengo ya Muda Mrefu

Mfano: Kununua duka lako mwenyewe badala ya kukodisha.

- Malengo yako ni ya aina gani? Ni ya matumizi au ni ya uwekezaji wako wa baadaye?
- Utahitaji shilingi ngapi ili kufanikisha malengo yako? Una mipango gani ya kupata hizo pesa? Umeshatengeneza bajeti ya kufuatilia?

# Kutengeneza Bajeti ya Kila Mwezi ya Familia

Sofia na Mateo wanafanya kazi dukani. Mateo ndiye mwenye duka. Wote wanapata mshahara kutoka dukani.

Wana familia ya watu watano; wana wasichana wawili, na mvulana mmoja. Watoto wao wanasoma shule na wanacheza michezo.

**Sasa tuangalie bajeti ambayo Sofía ametengeneza ya familia yake...**



# Kutengeneza Bajeti ya Kila Mwezi ya Familia

| MAPATO | | MATUMIZI | |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 6,000 | Mkopo wa Nyumba (duka + nyumba) | 10,000 |
| Mapato ya duka | 20,000 | Chakula | 2,000 |
| | | Afya | 500 |
| | | Shule | 1,000 |
| Gharama ya serikali ya kuhamisha pesa taslimu | 500 | Maswala ya shule | 1,000 |
| | | Matumizi (duka + nyumba) | 2,000 |
| | | Matumizi madogo yatakayojitokeza | 500 |
| **Jumla ya mapato** | **26,500** | **Jumla ya matumizi** | **17,000** |

***Akiba = Mapato – Matumizi = 26,500-17,000 = 9,500***

- Sasa, fanya bajeti yako.
- Jaribu kuhakikisha kwamba matumizi yako hayapiti kiwango cha mapato yako.
- Ikiwa matumizi yako ni zaidi ya mapato yako, unahitajika:
  - kupunguza matumizi.
  - kuongeza matumizi yako.

**Unahitaji baadhi ya mifano ya bajeti? Tembelea hiki kiunganishi ili kupakua baadhi ya mifano ya kufanya bajeti ya bure kutoka Google.**




Je, unatambua vyema matumizi yako?

Uliona matumizi yoyote ambayo ungetaka kupunguza?

Unaweza kuweka akiba ya shilingi ngapi?

Utafanyia nini akiba yako utakayokuwa umekusanya?

**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

# Kufanya bajet na Hey Sister




## Masomo ya Hey Sister

**Somo la 18: Ni vipi nyumba yangu inaweza kusimamia fedha zetu vyema?**

# SEHEMU YA 4: UWEKEZAJI

## Malengo:

1. Jifunze tofauti ya akiba na uwekezaji.
2. Kuelewa jinsi uwekezaji unaweza kukusaidia kutengeneza mapato ya biashara yako.



# Sasa Tuzungumze Kuhusu Uwekezaji

**Uwekezaji ni mchakato wa kutumia pesa kununua kitu ambacho kinaweza kuongezeka thamani.**

Unaweza kuwekeza kwa kununua mali, kama vile duka, au kuwekeza katika vifaa vya kifedha (kama vile bidhaa za dukani au bondi) vinavyotoa mapato lakini yenye baadhi ya hatari.

**Uwekezaji unaweza kukuletea mapato kwa njia moja kati ya mbili:**

Ukiwa umewekeza kwenye mali inayouzika, unaweza kupata pesa kwa kuiuza kwa faida au kwa kuikodisha.

Ukiwekeza kwenye vifaa vya kifedha, utapata mapato wakati bondi zitakapolipiwa riba, au wakati kampuni unayonunua bidhaa kwao kufanya vizuri kibiashara.

# Uwekezaji na Akiba

## Uwekezaji unatofautiana vipi na akiba?

Tofauti kubwa kati ya akiba na uwekezaji ni kiwango cha hatari.

Akiba huwa salama kuliko uwekezaji, Lakini uwekezaji unakupa uwezo wa kupata mapato zaidi kuliko akiba.

**Unahitajika kuzingatia akiba ikiwa….**

- bado huna hazina ya akiba ya dharura.
- utahitaji hizo pesa miaka kadhaa ijayo.
- una deni la kulipa.

**Unahitajika kuzingatia uwekezaji ikiwa…**

- umeshatengeneza hazina ya akiba ya dharura.
- una msimamo thabiti na imara wa kuingiza mapato.
- huna madeni yenye kiwango cha juu cha riba.



# Naweza Kuwekeza Kwenye Nini?

Sasa tuangalie baadhi ya mawazo ambayo wewe kama mjasiriamali, unaweza kuwekeza kwayo!



## Mtu Mwenyewe

Uwekezaji kwenye ujuzi wako ni mojawapo ya mambo bora sana unayoweza kufanya kama mjasiriamali. Unaweza kujiunga kwenye kozi zinazohusiana taaluma yako au kufanya program za mafunzo (kama hii hapa!)

## Mali

Ikiwa hujapanga kuhamisha biashara yako hivi karibuni, zingatia uwekezaji kwenye mali kwa biashara yako. Kununua mali kunaweza kukusaidia kwenye gharama ya kodi.

## Fedha Zako

Kuna njia nyingi za uwekezaji wa kifedha, kama vile bidhaa za dukani na bondi. Unaweza pia kuwekeza kwenye mshauri wa kifedha ili kukuongoza kwenye mikakati ya uwekezaji wa kifedha.






## Duka lako

Ikiwa ni vigumu kuendesha duka lako mwenyewe au ikiwa unataka kuuza bidhaa zaidi, zingatia uwekezaji kwenye wafanyikazi wa duka lako! Kuongeza mikono ya ziada kunaweza kukusaidia kuuza bidhaa zaidi na vitu, ambavyo vinaweza kutengeneza faida ya duka lako.

# SEHEMU YA 5:
# BIMA




## Malengo:

1. Kuelewa maana ya bima.
2. Kujifunza kuhusu aina tofauti za bima.
3. Kuangalia gharama na faida za bima.

# Sasa Tuzungumze Kuhusu Bima

**Una wasiwasi gani mkubwa wa Kifedha?**

**Unapanga vipi kuhusu matukio usiyoyatarajia?**

**Matumizi ya afya?**

**Limbikizo la deni?**

**Kifo cha wenye mapato?**

**Wizi wa dukani?**

## Zingatia bima.

Bima inatoa kinga ya kifedha dhidi hasara usizozitarajia au matumizi usiyoyatarajia.

Kuna aina mbili kuu za bima:

1. Bima ya Maisha
2. Bima ya Jumla

# Bima ya Maisha



Bima ya maisha inalipa wanafamilia wenye hati ya bima (waliokatiwa bima) baada ya kifo chao. Malipo hutolewa kwa mtu aliyeandikwa kwenye bima kama “mnufaika”

Wakati unanunua hati ya bima ya maisha, aliyekatiwa bima anaweza ima kulipa jumla ya pesa zote au kulipa kila baada ya muda, malipo yanayoitwa malipo ya kulipia bima, yanayolipwa kampuni inayotoa bima. Alafu Kampuni inayotoa bima inaahidi kulipa kiwango cha uhakika kwa aliyekatiwa bima wakati utakapofika muda wake, au kwa mnufaika ikiwa aliyekatiwa bima amekufa au kupatwa na ulemavu.

# Bima ya Jumla



Bima ya jumla ni mkakati wa kusimamia hatari inayotoa fidia ya kifedha ikiwa kutatokea hasara yoyote isiyokuwa kifo. Inajumuisha hasara au uharibifu wa mali na vilevile madeni.

Kampuni ya bima inaahidi kulipa kiwango cha uhakika kwa aliyekatiwa bima ili kufidia hasara zilizopatikana.

Baadhi ya mifano ya bima ya jumla ni pamoja na bima ya afya, gari, duka, kilimo, na usafiri.

# Mifano ya Bima ya Jumla



## BIMA YA DUKA

Bima ya duka inakinga biashara yako dhidi ya hatari kama vile wizi, moto, au ajali. Bila ya kuwa na bima ya duka, unaweza kuhitajika kulipa gharama za uharibifu na madai ya bima kutoka kwa mfuko wako.

## BIMA YA AFYA

Bima ya afya inashughulikia sehemu au afya yako yote na gharama za matibabu. Bima hii inaweza kushughulikia matukio ya afya makubwa na madogo. Bima ya afya inafanya kama net ya usalama wako na familia.

# Mambo ya Kuzingatiwa Kuhusu Bima

Unaweza kulipia malipo ya bima ya kiwango cha juu au chini kulingana na mpango wako wa bima. Pia, huduma nyingi za bima, hutapata malipo yako uliyolipia bima hata ikiwa hakuna matukio yoyote yaliyotokea yasiyokuwa yemetarajiwa au ajali.

Sio hatari zote zinazoweza kushughulikiwa na bima, au hata kupangia, sababu ambayo huwa ni muhimu kuwa na akiba. Wakati unaamua ikiwa unataka kuongeza bima, unaweza kuzingatia yafuatayo:

1. **Hatari:** Uwezekano wa kutokea hatari hiyo? Ikiwa hatari ilitokea, ni shilingi ngapi utapoteza, na ni shilingi ngapi utahitaji?
2. **Huduma za bima:** Kinachoshughulikiwa na huduma hiyo? Una uwezo wa kulipa malipo ya bima? Ni shilingi ngapi utalipwa ikiwa ajali itatokea? Je, unakumbana na hatari zingine ambazo hazishughulikiwa na huduma ya bima?



**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

# Bima na Hey Sister




## Masomo ya Hey Sister

**Somo la 17: Nahitajika ninunue bima?**

# SEHEMU YA 6: MKOPO

**Malengo:** Kuwa na ufahamu wa mkopo, sheria za mikopo, na jinsi ambavyo mkopo unaweza kutumiwa kwenye biashara.



# Mkopo ni Nini?



**Mkopo** maana yake ni kukopeshwa pesa na mtu – unaitwa mtaji – kwa kumuahidi kuwa utamlipa, kwa kawaida huwa na riba.

**Riba** ni gharama ya kukopeshwa pesa na mtu.

Kiwango cha riba kinapokuwa juu, utalipa kiwango cha jumla cha juu ili kununua kitu kwa mkopo.

Faida kubwa ya kutumia mkopo ni kuwa inakuruhusu kununua kitu – kama gari au nyumba – **bila ya kulipia pesa zote kwa wakati mmoja.**

# Jukumu la Mkopo kwenye Biashara

**Mkopo wa biashara unakupa nafasi ya kupata vitu ambavyo unahitaji kukuza biashara yako.**

Biashara ambayo haiwezi kukopa haitaweza kununua bidhaa au kulipa wafanyikazi inaohitaji kutengeneza bidhaa na faida.

Mkopo pia unafanya biashara zinaweza kuwekeza zinapopataka. Vitu kama muundomsingi wa duka lako ni ghali sana kwa watu wengi kulipia kwa wakati mmoja. Lakini ukiwa na mkopo, inawezekana kulipa baada ya muda, wakati unaendelea kutumia bidhaa na huduma muhimu wakati unazihitaji.



# Kwanini Ukope na Wakati wa Kukopa

- Unakopa pesa ikiwa matumizi yako yanazidi mapato yako au wakati kuna dharura.
- Pia unakopa wakati unahitaji pesa za kazi ya kushughulikia biashara au kuwekeza.
- Kosa la kawaida ambalo watu hufanya na mikopo ni kuwa wanaitumia kwa utumiaji wao, kama vile kuandaa karamu za kifahari au kununua bidhaa zao za gharama kubwa. Ikiwa ni lazima kutumia pesa kwa vitu hivi, basi matumizi yake yatokane na mapato yako au kwenye akiba. Unatakiwa ujiepushe kuchukua mikopo ya kufanikisha matumizi haya.
    - **Kwa mfano,** unaweza kuchukua mkopo kununulia jokofu la dukani kwako ambalo litakuruhusu kuweka aina mpya ya bidhaa wanazohitaji wateja, kama vile vinywaji baridi, aiskrimu, na vitu vya maziwa. Utaweza kuongeza mauzo yako na mapato halisi, na kupata faida ambayo itakuwezesha kulipa deni.


Sasa tujadili!
Kuna yeyote hapa amechukua mkopo? Kwanini ulichukua mkopo? Nani alikupa mkopo?
Wakati ulichukua mkopo, ulitia sahihi stakabadhi? Ulisoma stakabadhi ulizotia sahihi?
Ikiwa unasita kuchukua mkopo, tuambie kwanini?

# Sasa Tuzungumze Kuhusu Mikopo

- Mkopo huchukuliwa chini ya baadhi ya masharti na miongozo. Miongozo hii inaelezea yanayohitajika kati ya mkopi (wewe) na mkopwa.
- Ni muhimu sana kuhakiki masharti ya mkopo kabla ya kutia sahihi.
- Kwanza, unafaa kujua wajibu wa malipo yako kisheria ni upi. Utahitaji kujua ikiwa malipo ya mkopo wako yanalipwa tarehe maalumu kila mwezi ili kuepuka kuchelewesha malipo.
- Kuelewa masharti ya mkopo kunaweza kukusaidia wewe kujua ikiwa mkopo unakufaa kabla ya kuingia mkataba wa kulipia na mkopwa. Ikiwa kuna kitu kwenye masharti ya mkopo ambacho hukubaliani nacho, kama vile ada ya adhabu, unaweza kukataa mkopo huo.

# Masharti ya Mkopo

Wakati unaomba mkopo, mkopwa anafaa kuelezea bayana masharti ya mkopo kabla ya kukamilisha mkataba wowote wa ukopaji.

Ni muhimu kuhakiki masharti ya mkopo vizuri ili kuangalia vifungu vyovyote ambavyo vimefichika au ada ambayo yanaweza kukugharimu pesa.



**“Masharti ya Mkopo” ni sheria na masharti yanayohusishwa wakati wa kukopa pesa.**

Haya yanajumuisha:

- Muda wa kulipia mkopo na marudio ya ulipaji.
- Kiwango cha riba na ada zinazohusiana na mkopo.
- Kiwango unacholipa kila wakati unapofika wa kufanya malipo yako.
- Ni shilingi ngapi utalipia kwa jumla ukilinganisha na kiwango kamili cha mkopo unachopata.
- Ada za adhabu.
- Na hali yoyote maalum inayoweza kutumika.

# Mambo Makuu ya Kuzingatiwa Kutoka kwa Hii Moduli



1. **Fanya utafiti wako wakufaa.** Kuna aina nyingi sana za akaunti za akiba, bidhaa za mkopo, mikopo, na mipango ya bima kwenye soko. Kufanya utafiti wa kila bidhaa ya kifedha au huduma unayotazamia, kutakusaidia kuchagua ambayo inakufaa wewe.
2. **Soma stakabadhi kwa makini.** Kutumia bidhaa na huduma za kifedha kunamaanisha kusoma na kutia sahihi stakabadhi nyingi. Kabla hujatia sahihi chochote, hakikisha kuwa unasoma stakabadhi kwa umakini. Stakabadhi hizi zitakuelezea taarifa muhimu kuhusu sheria na masharti ya bidhaa au huduma unayochagua.
3. **Fikiria kuhusu mustakabali wa biashara yako.** Kuna aina tofauti za bidhaa na huduma za kifedha zilizotengenezwa maalum kusaidia kulinda au kukuza biashara yako. Wakati unazingatia mkopo au kuwekeza, fikiria kuhusu malengo ya baadaye ya biashara yako, na jinsi ambavyo bidhaa hizi zitakusaidia kufikia hayo malengo.
4. **Imarisha uhuru wa kifedha.** Kufungua akaunti yako mwenyewe ya kifedha, kuchagua mpango wa bima, na kufanya bajeti kutakusaidia wewe kuwa na uhuru wa kifedha. Unakuwa unafanya maamuzi yako mwenyewe kuhusu fedha zako binafsi za biashara.




Una mashaka yoyote na maswali?

Uliza tu!

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

STRATEGIC IMPACT ADVISORS



www.siaedge.com
Laini ya Pili
Laini ya Tatu

